**Learning by Ear – Hygiene: How to avoid diarrhoea**

**Episode 08** **“Shule ndiyo mambo yote”**

**Author:** **Njoki C. Muhoho**
**Medical Advisor** **Dr Ng’ethe Muhoho**
**Editor** **Maja Braun**
**Kisuaheli** **Eric Ponda**

| Scene | Characters | |
|---|---|---|
| **1** | 1. SAM<br>2. CHEMU<br>3. NARRATOR | **SAM – 17, m.** |
| | | **MARIA – 43, f.** |
| **2** | 1. SAM<br>2. CHEMU | **EDITH– 40, f.** |
| | | **EDDI – 36, m.** |
| **3** | 1. SAM<br>2. CHEMU<br>3. EDDI | **DR SALLY – 34, f.** |
| | | **CHEMU – 15, f.** |
| **4** | 1. SAM<br>2. CHEMU<br>3. NARRATOR | **NARRATOR** |

**INTRO**

**MUSIC: THEME MUSIC**

**01. NARRATOR** HUJAMBO NA KARIBU KWA SEHEMU YA NANE YA MFULULIZO WA VIPINDI VYA NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO.INAYOZUNGUMZIA MASUALA YA USAFI NA KINGA DHIDI YA UGONJWA WA KUHARA.KATIKA KIPINDI KILICHOTANGULIA SAM NA CHEMU WALIWAFAFANULIA MAMA ZAO UMUHIMU WA USAFI WAKATI WA MAANDALIZI YA CHAKULA; NA WAO PAMOJA NA WANAFUNZI WENZAO WALIANDAMANA HADI HOSPITALINI KUPIMWA ILI KUBAINI IWAPO WANA CHANGO VIDUDU AU VIMELEA VINAVYOSABABISHA UGONJWA WA KUHARA..

SASA TUUNGANE NAO TUZISIKIE JUHUDI ZAO SHULENI ZA KUPAMBANA NA KUENEA KWA UGONJWA WA KUHARA, MOJA YA MARADHI YANAYOSABABISHA VIFO VINGI VYA WATOTO BARANI AFRIKA.

**SCENE 1: SECONDARY SCHOOL**

**02. SFX SCHOOL PLAY GROUND NOISES**

**03. SAM** ***(shouting over the noise)*** Chemu… Chemu….njoo kwa hapa..!

**04. CHEMU** ***(excited)*** Sam! Unafanya nini hapa shuleni kwetu?. Unapaswa kuwa shuleni kwenu.

**05. SAM** ***(Closer)*** Nimekuja kukuona …! Unajua …! Nimetoka msalani kwetu …! na nina wasiwasi sana.

**06. CHEMU** Wasiwasi wa nini sasa…? Uko salama…? Au umeanza kutoa minyoo tena?

**07. SAM & CHEMU *(laughing at the joke)***

**08. SAM** Wacha masihara…….!. mimi nimepona kabisa sasa.!

**09. CHEMU** Sasa chooni kuna nini….? Nafahamu.. nafahamu vyema misala yetu ilivyo….!.

**10. SAM** Nzi…!

**11. CHEMU** ***(firmly)*** Ndio ….. kuna nzi wengi sana kila mahali msalani. Nzi kwenye shimo la choo, kutani, nje na hata wanazirukia nguo zetu... nzi…. Nzi… kila mahali. Mabuu, makombamwiko na kila aina ya wadudu….

**12. SAM** Na unajua nini Chemu…? Vyoo hivyo haviko mbali sana na eneo tunako kula chakula.

**13. CHEMU** Kweli!

**14. SAM** Nimekuwa nikiyatafakari yale yote tuliyofunzwa na mjomba Eddi kuhusu ugonjwa wa kuhara,vimelea na mayai ya vidudu hivyo tumboni vinavyosambazwa na nzi hawa.

**15. CHEMU** Lazima tutafute suluhu.

**16. SAM** Na kisha suluhisho la haraka. Naihofia afya ya kila mmoja wetu hapa shuleni. Na siku zote hizo tumekuwa tukiishi katika mazingira haya na tishio la kuambukizwa pasi na kujua!!

**17. CHEMU** Naihofia sana familia yangu, marafiki na watu wote tunaotangamana shuleni …..!

**18. SAM** ***(sadly)*** Nina wasi wasi Chemu, huwezi kujua…!,labda mimi ndiye niliyemsambazia mdogo wangu Fatu vimelea vilivyokuwa vyooni…!.

**19. CHEMU** ***(warmly comforting)*** La hasha…..! usiwe na fikra hizo…!. Pengine Fatu alivipata vimelea hivi kutoka … kutoka mahali kwengine kokote, hata labda kwenye matunda ya sokoni.Pengine yeye ndiye aliyekuambukiza ugonjwa huu……..

**20. SAM** Hmm….. Suala hilo halinitoki akilini kila wakati !

**21. CHEMU** Tusahau yaliyopita na tugange yajayo…! Mungu ailaze roho ya Fatu mahali pema peponi…

**22. SAM** **(*happier*)** Tulitimize hili kwa heshima ya marehemu Fatu!

**23. CHEMU** Nini?

**24. SAM** Kusafisha vyoo... wacha wazimu...! Hilo ndilo suala tunalolijadilia hapa…! Tukutane msalani baada ya masomo…Sawa Chemu?

**25. CHEMU** Kwenye vyoo vyetu?

**26. SAM** Ndio... kwanza tufanye.. ehhh.. kwanza tuitathmini kazi yote inayohitajika kufanywa.. kisha…....

**27. *SFX BELL RINGS***

**28. SAM** Kengele ndio hiyo imelia

**29. CHEMU** Tuonane baada ya masomo

**30. SAM** Haya tukutane huko msalani.

**31. NARRATOR** KWA MARAFIKI HAWA WAWILI MKUTANO WAO HUKO MSALANI SI JAMBO LA KUSISIMUA. HATAHIVYO WAKO MSTARI WA MBELE KUZITAMBUA TAHADHARI NA NJIA BORA ZA KUJIKINGA NA MARADHI YA KUHARA. HEBU TUSIKILIZE IWAPO JUHUDI ZAO ZITAFANIKIWA WAKATI WATAKAPOKUTANA CHOONI BAADA YA MASOMO...

**SCENE 2: AT THE PIT LATRINES**

**32.** ***SFX: MANY FLIES BUZZING. A DOOR CREEKS PAINFULLY. FLIES BUZZ GETS EVERY LOUD AND CONTINUES***

**33. CHEMU** Oh jamani kweli hili ni eneo limevamia na nzi .. Hebu tazama .. wako kila mahali…

**34. SAM** Sakafuni,…kutani, …kwenye dari… na hata kwenye nguo zetu…

**35.** ***SFX: RUSTLE OF CLOTHES***

**36. CHEMU** ***(panic)..*** Ooh no..nendeni huko nendeni … nzi wachafu. Mtaniambukiza kuhara.

**37. SAM** (***laughing***) Unaongea na nzi…? hawawezi kukusikia…! Labda tuwafukuze...

**38. CHEMU** Vipi?

**39. SAM** Nadhani tunahitaji msaada wa mjomba Eddi. Yeye ni afisa wa huduma za afya ya jamii, kwani umesahau?Atajua la kufanya.

**BRIDGE MUSIC**

**<u>SCENE 3: SCHOOL LATRINES</u>**

**40. NARRATOR** AMA KWA HAKIKA SIKU ILIYOFUATIA MJOMBA EDDI ALIANDAMANA NAO HADI SHULENI.KWAVILE YEYE NI AFISA WA HUDUMA ZA AFYA YA JAMII, EDDI ALIKUWA TAYARI KUWASAIDIA VIJANA HAWA**.**

**41.** ***SFX: MANY FLIES BUZZING. A DOOR CREEKS PAINFULLY. FLIES BUZZ GETS VERY LOUD AND CONTINUES***

**42. EDDI** Oh, oh oooh oohh, sasa naelewa mulichokuwa mukimaanisha.....! Hapa ndipo magonjwa yanapoanzia...!.Kiasi cha wanafunzi wangapi wanaitumia misala hii?

**43. SAM** Mia tatu kutoka shuleni kwetu…!

**44. CHEMU** Na wengine wengi kutoka shule ile nyingine… **(spits loudly)** Nusura nimmeze nzi mmoja... hebu tutoke hapa.

**45. SAM** Kweli hatuwezi kuendelea kukaa hapa, kuna harufu mbaya sana…!.

**46.** ***SFX: CREEKS AS DOOR CLOSES. FLY BUZZ DIES OFF***

**47. CHEMU** Afadhali hapa.. naweza kufungua mdogo nikiongea sasa!

**48. EDDI** Kweli pale ndani pako hali mbaya sana . Hebu fikirieni itakavyokuwa ,endapo nusu ya wanafunzi hawa wanaambukizwa na kisha waende majumbani mwao na kuziNAYOZUNGUMZIA MASfamilia zao? Unadhani ni watu wangapi watakuwa wameambukizwa katika kipindi cha kama miezi miwili?

**49. SAM** ***(worried)*** Tsk..Tsk…Tsk .. hali hii ni hatari kwelikweli.

**50. CHEMU** Kweli kabisa.Hebu twambie Mjomba Eddi, mtu anapoambukizwa ugonjwa na nzi hawa, jee ataugua mara moja au mtu anaweza kuambukizwa vimelea na kisha akaendelea kuwa na afya nzuri?

**51. EDDI** Sio hapo kwa papo.Hilo linachukua kiasi cha siku kati ya 4-7. Inategemea na Mtu binafsi na hali yake ya afya,uwezo wa mwili wake kupambana na maradhi na masuala mengine mengi. Lakini watoto huathirika haraka zaidi.

**52. SAM** Kama yaliyomsibu Fatu.

**53. EDDI** Ndio kama ilivyotokea kwa marehemu Fatu.

**54. CHEMU** Lazima tutafute njia ya kuikomesha hali hii.Mjomba Eddi tutawezaje kuwazuia nzi hawa wote? Hatuwezi kuvifunga hivi vyoo.Wanafunzi wanavihitaji.

**55. EDDI** Tunaweza kuishauri Shule kuhusu njia bora ya usimamizi wa vyoo hivi.

**56. SAM** Vyoo vinapaswa kusimamiwa vipi?

**57. EDDI** Kwanza kabisa vyoo vinapaswa kuoshwa zaidi ya mara moja kwa siku. Watu wanaovisafisha lazima wawe na mavazi ya kujilinda.……kama vile glavu.

**58. CHEMU** Jee kama maji hayapo?. Aghalabu maji hayapo shuleni kila wakati.

**59. EDDI** Shule nyingi hazina maji ya kuaminika.Katika hali hiyo sharti muinyunyizie jivu sakafu ya vyoo.

**60. SAM** Jivu… unamaanisha jivu la Moto? Hii inanikumbusha ndizi za shangazi Maria alizozichoma kwenye jivu wakati mimi na Fatu tulipokuwa wagonjwa.!Una uhakika?

**61. EDDI** Sam hata hivyo, ndizi hizo hazingekusaidia kwa vyovyote. Lakini hapa jivu hilo litasaidia sana…! Unajua baadhi ya hivi vyoo havina sakafu ya simiti.Vile vilivyo na sakafu ya aina hiyo vinaweza kuoshwa kwa maji kila wakati.

**62. CHEMU** **Na vile ambavyo havina sakafu hiyo?**

**63. EDDI** Hapo ndipo jivu huwa na manufaa makubwa. Unanyunyuzia jivu hilo sakafuni wakati wa usiku na kufagia asubuhi bila shida.

**64. SAM** Kwanini tutumie jivu?

**65. EDDI** Jivu huua nzi na mabuu, na hivyo kupunguza idadi ya wadudu hao.Lakini ni lazima vyoo hivyo vifagiliwe kabla ya kuanza kutumiwa. Maana wakati jivu hilo linaposhika maji maji ya mkojo, basi ni rahisi sana kwa vidudu kuanza kusambaa tena. Hivyo lazima tuwe waangalifu sana.

**66. CHEMU** Unamesema ni lazima tuoshe sakafu zilizowekwa simiti. Mara nyingine hatuna maji ya kutosha.

**67. EDDI** Ningependekeza kila mwanafunzi alete chupa ndogo ya maji kutoka nyumbani ili mahsusi kwa shughuli hiyo.Kisha tunaweza kuosha vyoo kwa kutumia fagio ndefu na kuipiga deki sakafu kwa fagio tamvua.

**68.** **CHEMU** Fagio tamvua..?

**69.** **EDDI** Ndio,lakini fagio hizo sharti zisikamuliwe kwa mikono! Na jambo jingine, ni lazima sehemu ya choo iliyowazi ifunikwe kila mara wakati hakitumiki.

**70.** **SAM** Lakini Mjomba Eddi tutaweza kufunika vipi choo hicho.?

**71.** **EDDI** Tutaiomba shule itengeneze vifuniko vya mbao vilivyo na mipini mirefu. Ni rahisi kuitengeneza **na si ghali.**

**72.** **SAM** Kumbe…! Uncle Eddi kumbe bado kuna mengi ya kujifunza.

**73.** **CHEMU** Sasa kichwa changu kimeanza kuniuma kwasababu ya maelezo yote haya niliyojifunza!.

**74.** **EDDI** Ni kweli, lakini kuna mambo rahisi ambayo mtu anaweza kuyafanya kila siku maishani. Sasa twendeni tukazungumze na viongozi wa shule.

**75.** **CHEMU** Sawa.. Twendeni… ni huku…!

**76.** **EDDI** Lakini tumesahau jambo moja muhimu.

**77.** **SAM** Ni jambo gani hilo?.

**78. EDDI** Sehemu ya kunawa mikono karibu na vyoo hivi kila mara wanafunzi wanapotoka chooni. Na kama hakuna maji ya mfereji, shule inaweza kununua mitungi iliyo na mifereji kuweka maji ya kunawa. Mikebe yenye tundu pia inaweza kutumiwa iwapo mitungi hiyo haitapatikana.

**79. CHEMU** Mikebe inayovuja?

**80. EDDI** Ndio unatoboa tundu chini ya mikebe hiyo kwa kutumia msumari .Kisha mikebe hiyo inaning'inizwa chini ya mti karibu na vyoo hivyo.

**81. SAM** Lakini si maji yote yatamwagika.

**82. EDDI** Wazo zuri sana . Lakini unaweza kutumia kitu cha kuzibia kwa mfano vijiti vilivyochongwa sawia na ukubwa wa tundu lenyewe ili kuzuia maji hayo yasitoke wakati wote ila tu inapohitajika.Hali yenyewe ni kuwa unakiondoa kitu kile kinachoyazuwia maji,nawa mikono na kisha ukirejeshe.

**83. CHEMU** **(*laughing)*** Wazo zuri sana … Basi sote tunaweza kuimba ule wimbo wetu mpya kuhusu umuhimu wa kunawa mikono.**CHEMU HUMS THE 'WASH YOUR HANDS SONG'**

**84. NARRATOR** NI JAMBO LA KUFURAHISHA KUONA MIKAKATI RAHISI INAVYOWEZA KUTUMIKA KUZUWIA MAJANGA YA KIAFYA. LAKINI HAYO YOTE YANAWEZA KUFAULU IWAPO YANAKUWA SEHEMU YA MAISHA YA KILA SIKU. ZAIDI YA YOTE URAFIKI WA SAM NA CHEMU UNAZIDI KUIMARIKA, NA UNA MANUFAA SIO TU KWAO PEKEE BALI KWA JAMII NZIMA. BILA SHAKA HALI YA USAFI ITAIMARIKA SHULENI NA HATA MAJUMBANI KWASABABU YA JUHUDI ZAO.

KWELI VIJANA HAWA WAMEKUWA MABALOZI WA MASUALA YA USAFI.JEE SAFARI YAO INAYOENDELEA ITATUPELEKA WAPI? UNGANA NASI TENA KWA MAKALA NYINGINE IJAYO YA NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO ILI UJIFUNZE MENGI TU KUHUSU MASUALA YA USAFI. KWA MAELEZO ZAIDI, HADITHI FUPI AU HATA UKITAKA KUTUMA MAONI TEMBELEA MTANDAO WETU WA WWW.DW-WORLD.DE/LBE. **HADI WAKATI MWENGINE, KWA HERI KWA SASA.**